# JARIDA la eGA

## Mamlaka ya Serikali Mtandao

Toleo la 8 | Aprili - Juni 2024

# e-Mrejesho YASHINDA TUZO UMOJA WA MATAIFA




- Umetambuliwa na umoja huo kama jukwaa linalowezesha serikali kukusanya maoni na malalamiko ya wananchi kwa njia ya kidijitali
- Tuzo hiyo imetolewa Juni 26, 2024 nchini Korea ya Kusini

# Yaliyomo

Kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu....1

e-Mrejesho yashinda tuzo Umoja wa Mataifa....2

Bi. Zuhura Mwindi Mfanyakazi Bora e-GA ,2024....3

GMS yarahisisha mawasiliano Serikalini....4

Vijana leteni bunifu za TEHAMA zinazosaidia Serikali....5

Mfumo wa MGov 2.0 waboreshwa kuongeza ufanisi zaidi....6

Manispaa ya Tabora yaokoa Milioni 160 kupitia mfumo wa e-Board....8

GISP yaongeza ufanisi wa miradi ya TEHAMA....9

Wakaguzi wa ndani: Waaswa kuelimisha juu ya maendeleo ya TEHAMA....10

Manispaa ya Ilemela yafaidika na mfumo wa e-Board....11

Twiga Cloud: Mkombozi wa faili zako za kidijiti....12

e-GA na mkakati wa kukuza vipaji kwa vijana katika sekta ya TEHAMA ....12

Matukio katika picha ....15



## Kutoka Kwa Mkurugenzi Mkuu

Karibu katika toleo la nane la Jarida la Mtandaoni kutoka Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA). Katika jarida hili utasoma na kujifunza kuhusiana na kazi na huduma mbalimbali zinazofanywa na Mamlaka kama vile ujenzi wa mifumo inayoendana na mahitaji halisi ya Taasisi husika, utoaji wa huduma za ushauri na msaada wa kiufundi, uboreshaji wa njia za utoaji wa huduma za Serikali Mtandao, utengenezaji na uendeshaji wa mifumo na miundombinu ya TEHAMA Serikalini inayosaidia kuongeza ufanisi wa utendaji kazi Serikalini na utoaji wa huduma bora kwa umma.

Hali kadhalika, katika Jarida hili utaweza kufahamu juhudi na shughuli mbalimbali zinazofanywa na Mamlaka katika utekelezaji wa dhana ya Serikali Mtandao.

Toleo hili ni muendelezo wa matoleo mengine yaliyopita yanayokuhabarisha kuhusu jitahada za e-GA katika kukuza na kuchochea matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) Serikalini, kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma za umma na kuleta mabadiliko ya kijamii na kiuchumi.

Nichukue fursa hii kukukaribisha tena katika kurasa hizi ili upate kuifahamu vizuri e-GA na shughuli mbalimbali inazozitekeleza.

Nakutakia usomaji mwema.

Mhandisi Benedict B. Ndomba
Mkurugenzi Mkuu e-GA

# MFUMO WA e-Mrejesho WASHIDA TUZO YA UMOJA WA MATAIFA YA UBUNIFU KATIKA HUDUMA ZA UMMA




Tanzania imeshinda tuzo ya Umoja wa Mataifa ya Ubunifu katika Huduma za Umma kwa mwaka 2024 'UN Public Service Innovation Awards' kupitia mfumo wa e-Mrejesho, ambao umetambuliwa na umoja huo kama jukwaa linalowezesha serikali kukusanya maoni na malalamiko ya wananchi kwa njia ya kidijitali, na hivyo kufanya maamuzi ya sera na utekelezaji kwa wakati.

Hafla ya utoaji wa tuzo za Umoja wa Mataifa kuhusu Huduma za Umma imefanyika Juni 26 mwaka huu wakati wa kilele cha maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma ya Umoja wa Mataifa 'UN Public Service Week 2024' katika jiji la Incheon, Jamhuri ya Korea.

Tanzania ilikuwa moja kati ya nchi mbili tu za Afrika zilizotunukiwa tuzo hiyo, nyingine ikiwa ni Afrika Kusini ambapo jumla ya nchi 73 wanachama wa Umoja wa Mataifa zilishiriki na mifumo 400 iliwasilishwa wakati mifumo 15 pekee ndiyo ilishinda tuzo mbalimbali ukiwemo mfumo wa e-Mrejesho.

Tuzo hizo zilitolewa na Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa katika Idara ya Masuala ya Kiuchumi na ya Kijamii Bw. Li Junhua na kupokelewa na Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma Bw. Xavier Daudi.

Mfumo wa e-Mrejesho umesanifiwa na kutengenezwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, unaruhusu wananchi kuwasiliana na taasisi zote za Serikali na kuwasilisha maoni, malalamiko au pongezi.

Mkurugenzi Mkuu wa e-GA Mhandisi Benedict Ndomba amesema kuwa, tuzo hiyo inaonesha utambuzi wa mchango mkubwa wa mfumo wa e-Mrejesho duniani kama jukwaa huru linalowaunganisha wananchi na serikali katika kuboresha utawala wa demokrasia kupitia teknolojia.

Amebainisha kuwa, mfumo huu unaruhusu Serikali kukusanya malalamiko, maswali na maoni ya wananchi na kuyafanyia kazi kwa wakati na pia unamuwezesha mwananchi kutuma maoni yake bila kujulikana ikiwa mwananchi hatotaka kujulikana.

"Mfumo wa e-Mrejesho ni jukwaa huru kwani umezingatia faragha za wananchi ambapo kwa wale wasiopenda kujulikana wanapowasilisha maoni yao serikalini wanaweza kuwasilisha bila kujulikana, na hivyo kuhakikisha sauti za watu wote zinasikilizwa, hii inachochea utamaduni wa uwazi na uwajibikaji katika taasisi za umma", amesema Ndomba.

Ameongeza kuwa, mfumo wa e-Mrejesho ni hatua kubwa katika juhudi za e-GA za kujenga daraja kati ya serikali na wananchi wake na kuwa, ushindi wa tuzo hio kutoka kwa Umoja wa Mataifa unaonesha namna azma ya e-GA ya kukuza uwazi na uwajibikaji katika utawala wa umma kupitia teknolojia inavyotekelezwa.
"Mfumo wa e-Mrejesho unapatikana kwa njia tatu ambazo ni kupitia simu ya mkononi kwa kubofya *152*00# na kisha kuchagua namba 9 na kisha namba 2, njia zingine ni kupitia simu janja kwa kupakua Aplikesheni (Mobile App) ya e-Mrejesho inayopatikana kwenye Play Store na Apple Apps Store, na kwa njia ya Tovuti ya emrejesho.gov.go.tz", amesema Ndomba.

Aidha, amebainisha kuwa, ikiwa mwananchi atakosea kuwasilisha lalamiko lake katika taasisi husika, mfumo wa e-Mrejesho unaruhusu lalamiko hilo kuhamishwa kutoka taasisi moja kwenda taasisi nyingine, na pia unamruhusu mwananchi kukata rufaa kwenda ngazi ya juu ya taasisi ikiwa hatoridhika na majibu yaliyotolewa kuhusu lalamiko lake.

"Mfumo huu unasaidia kuongeza uwajibikaji, kwani lalamiko linapofika kwenye taasisi litaonekana kwenye ngazi zote za uongozi wa taasisi hiyo na kila Afisa aliyelifungua ama kulifanyia kazi ataonekana, pia mfumo unafanya uchambuzi wa taarifa na kumuwezesha Katibu Mkuu Ofisi ya Rais UTUMISHI na Katibu Mkuu Kiongozi kuona malalamiko yaliyowazi, yanayoshugulikiwa na yaliyokamilika kupitia 'dashboard' maalum", amesema Ndomba.

Machi 13 mwaka huu, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe.Dkt Samia Suluhu Hassan, aliwataka viongozi wa umma kutumia Mfumo e-Mrejesho ili kupokea maoni ya wananchi kuhusu Serikali na pia kutoa mrejesho kwa wananchi kupitia mfumo huo ili kuimarisha uwajibikaji kwa viongozi wa umma.

Dkt. Samia alitoa maelekezo hayo Ikulu jijini Dar es Salaam, mara baada ya kuwaapisha viongozi aliowateua katika nafasi mbalimbali wakiwemo Wakuu wa Mikoa, Katibu Mkuu, Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wa Halmashauri.

Tuzo za Umoja wa Mataifa kuhusu Huduma za Umma zinalenga kuhamasisha ufanisi, uwazi na ushirikishwaji katika kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa, na kuthamini mchango wa taasisi za umma katika kukabiliana na mahitaji ya kijamii, kiuchumi na mazingira ya jamii.

Wiki ya Huduma ya Umma ya Umoja wa Mataifa ni tukio la kila mwaka, linaloadhimishwa kimataifa kwa lengo la kusherehekea thamani na umuhimu wa huduma ya umma kwa jamii na hujadili jinsi ya kuboresha utoaji wa huduma kwa umma duniani kote.



# ZUHURA MWINDI
# MFANYAKAZI BORA WA e-GA MWAKA 2024

Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), imemtangaza Msaidizi wa Mtendaji Mkuu Bi. Zuhura Mwindi, kuwa mfanyakazi bora wa Mamlaka kwa mwaka 2024, baada ya kuibuka mshindi kwa kupata kura nyingi dhidi ya washindani wengine.

Uchaguzi wa mfanyakazi bora wa Mamlaka ulifanyika April 25 mwaka huu, baada ya kuwashindanisha wafanyakazi bora 10 kutoka katika Idara na vitengo na kisha Menejimenti kupiga kura ili kumpata mfanyakazi bora wa Mamlaka kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Akizungumza wakati wa zoezi la uchaguzi, Meneja Rasilimaliwatu na Utawala Bw. Erick Kalembo alisema kuwa, orodha ya wafanyakazi bora wa Idara na Vitengo ilipatikana baada ya kufanyika uchaguzi wa ndani kwa kila Idara na vitengo na kisha orodha hiyo kuwasilishwa Idara ya Huduma na Uwezeshaji (DCS).

"Baada ya idara ya DCS kupokea orodha hiyo tulifanya kikao na menejimenti na kupiga kura ya siri ili kupata mshindi wa taasisi", alisema Kalembo.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa e-GA Mha. Benedict Ndomba, alisema kuwa e-GA inatambua na kuthamini mchango wa watumishi wake wote katika kufikia malengo ya taasisi na kuwa, uchaguzi wa mfanyakazi bora ni motisha kwa wafanyakazi wote kuendelea kufanya kazi vizuri zaidi na kwa weledi.

"Watumishi wote wa e-GA ni bora na ndiomaana taasisi huweza kufikia malengo iliyojiwekea kila mwaka kwa mujibu wa mpango mkakati wa Mamlaka wa mwaka 2021/2022 – 2025/2026 kwani kila mtumishi hufanya kazi kwa bidii, hivyo niwapongeze sana watumishi wote wa e-GA" alisema Ndomba.

Aidha, Ndomba aliitaka Menejimenti kuwapima watumishi wote bora waliochaguliwa kwa kila Idara na Vitengo na kisha kupiga kura kwa uwazi na kumchagua mfanyakazi bora wa Mamlaka, kwa kuzingatia vigezo vilivyopo bila upendeleo wa aina yeyote.

Uchaguzi huo ulifanyika kwa njia ya mtandao 'online' kupitia Mfumo wa Kidijitali wa uendeshaji vikao wa e-Mikutano ambapo Menejimenti ilipiga kura na kupata wafanyakazi bora watatu (3) walioingia tatu bora na hatimaye kumpata mfanyakazi bora wa taasisi.

Walioingia tatu bora ni Bi. Zuhura Mwindi aliyeshika nafasi ya kwanza akifuatiwa na Afisa TEHAMA Darwin King'ani kutoka Idara ya Huduma za TEHAMA na Afisa TEHAMA Stanslaus Kayombo kutoka Idara ya Miundombinu na Uendeshaji aliyeshika nafasi ya tatu.

Naye Mfanyakazi bora wa Mamlaka kwa mwaka 2024 Bi. Zuhura Mwindi, aliishukuru Mamlaka kwa kumchagua na kutambua jitihada zake katika utendaji kazi na kwamba ushindi huo umeongeza chachu ya kufanya kazi kwa ufanisi na bidii zaidi.


Aidha, Bi. Zuhura aliwashukuru watumishi wa Idara ya Huduma za Uendeshaji kwa ushirikiano na kutambua mchango wake katika Idara uliopelekea kuibuka mshindi wa Idara hiyo na hatimaye kuwa mfanyakazi bora wa taasisi.

"Ninaishukuru sana Menejimenti na watumishi wenzangu wa e-GA kwa kutambua na kuthamini jitihada zangu, niwatie moyo watumishi wenzangu kuendelea kufanya kazi kwa bidii na kwa kujituma ili kuweza kufikia malengo ya Taasisi" Alisema Bi. Mwindi.

**"Tumepokea orodha ya wafanyakazi bora kutoka kila Idara na Vitengo ambapo watumishi wa maeneo husika walipiga kura huru na sasa ni wakati wa sisi Menejimenti kupiga kura ili tuweze kumpata Mfanyakazi bora wa taasisi "**

Bw. Erick Kalembo
Meneja wa Utawala na Rasilimaliwatu






# GMS YARAHISISHA MAWASILIANO SERIKALINI

Mawasiliano kwa njia ya baruapepe 'email', yameendelea kushika hatamu duniani ikiwa ni miongoni mwa njia ya haraka ya mawasiliano inayotumika katika uendeshaji wa shughuli mbalimbali za taasisi.

Kukua kwa matumizi ya baruapepe, kunatokana na ukuaji wa teknolojia na hivyo, kuwa ni moja ya njia ya haraka na inayoaminika katika mawasiliano rasmi ya kiofisi.

Ili kuhakikisha Serikali inapiga hatua katika matumizi ya baruapepe, Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) imetengeneza Mfumo wa baruapepe Serikalini (Government Mail System - GMS), ili kurahisisha mawasiliano na kubadilishana taarifa ndani na nje ya Serikali kwa uhakika na usalama zaidi.

Meneja wa Utengenezaji wa Mifumo ya TEHAMA wa e-GA Bw. Abdallah Samizi alisema, e-GA ilitengeneza mfumo wa GMS mwaka 2013 ili kuhakikisha Serikali inakuwa na mfumo salama na wa uhakika katika mawasiliano yake.

"Awali, kabla ya kuwepo kwa mfumo huu wa GMS, taasisi za Serikali zilitumia mifumo yake binafsi iliyotengenezwa na wakandarasi au baruapepe za muda mfupi 'disposable email' kama Yahoo na Gmail kubadilishana taarifa na nyaraka mbalimbali za Serikali", alifafanua Bw. Samizi.

Alibainisha kuwa, mifumo hiyo ilikuwa ikifanya kazi kwa kusuasua kutokana na changamoto mbalimbali za kimiundombinu na pia haikuwa salama kwasababu hakuna uhakika wa mahali zinapotunzwa taarifa kwani hakuna makubaliano na Serikali.

Aidha, aliongeza kuwa gharama za ununuzi na uendeshaji wa mifumo hiyo ya baruapepe zilikuwa kubwa na ufanisi wake ulikuwa mdogo, changamoto ambazo zimetatuliwa kupitia mfumo wa GMS ambao umeimarisha usalama wa taarifa za Serikali na uhakika wa upatikanaji wa huduma ya baruapepe.

"GMS ina usalama wa kutosha kwa kuhakikisha mawasiliano yote kwa njia ya baruapepe yanahifadhiwa na kubaki kwenye miundombinu ya Serikali na hivyo kuwa na uhakika wa usalama wa taarifa za Serikali", alisisitiza Bw. Samizi.

Aliongeza kuwa, mfumo wa GMS ni shirikishi na unawezesha mawasiliano na ubadilishanaji wa taarifa na nyaraka baina ya taasisi moja na nyingine, hivyo kuipunguzia Serikali gharama za ununuzi na uendeshaji wa mifumo ambapo awali Serikali ilitumia fedha nyingi katika kuhudumia mifumo mbalimbali ya baruapepe katika taasisi za umma.

**"Taasisi za Umma zinatumia rasilimali shirikishi katika kuendesha mfumo huu ikilinganishwa na hapo awali ambapo, kila taasisi ya umma ilijaribu kutengeneza mfumo wake wa kipekee uliotumia gharama nyingi za uendeshaji na haikufanya kazi kwa ufanisi wala kukidhi mahitaji halisi ya mtumiaji"**

Bw. Abdallah Samizi.
Meneja wa Utengenezaji wa Mifumo ya TEHAMA

Alibainisha kuwa, mfumo wa GMS ni wa kuaminika kwani umetengenezwa nchini na wataalamu wa ndani, hivyo taarifa na nyaraka mbalimbali za Serikali zinapotumwa hazitoki nje ya Tanzania.

Alisisitiza kuwa, taarifa zinazotumwa kupitia GMS zinahifadhiwa mahali salama kwenye vituo vya Serikali vya kuhifadhi mifumo na taarifa na hivyo kudumisha usiri wa taarifa hizo na kulinda maslahi mapana ya taifa.

"Tofauti na mifumo mingine ya baruapepe, mfumo huu wa baruapepe Serikalini (GMS) umeunganishwa na mifumo mingine na hivyo kurahisisha utumiaji wa mifumo mingine ndani ya Serikali", alisema Bw. Samizi na kuongeza kuwa,

"Mfumo wa GMS umeendelea kuboreshwa kila wakati kulingana na mabadiliko ya ukuaji wa teknolojia yanayojitokeza mara kwa mara ili kukidhi viwango stahiki vya mifumo ya baruapepe duniani".

Bw. Samizi alibainisha kuwa, matumizi ya mifumo ya baruapepe isiyo ya Serikali inahatarisha usalama wa taarifa za Serikali na hivyo, ni wajibu wa watumishi wa umma kulinda usalama wa taarifa za Serikali kwa kufanya mawasiliano na kutuma nyaraka za Serikali kupitia GMS.

Hadi sasa taasisi za umma 690 zinatumia mfumo huu wa GMS katika mawasiliano ya kiofisi kwa usalama na uhakika, pia mfumo huu unatoa fursa kwa taasisi za umma, kuweka matangazo na matukio mbalimbali ya kitaifa kwenye ukurasa wa mbele wa mfumo huu tofauti na mifumo mingine ya barua pepe.




# VIJANA LETENI BUNIFU ZA TEHAMA ZINAZOISAIDIA SERIKALI

Meneja wa Kituo cha Utafiti, Ubunifu na Uendelezaji wa Serikali Mtandao (eGOVRIDC) cha Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Dkt. Jaha Mvulla, amewata vijana watafiti na wabunifu kwenye eneo la TEHAMA kuwasilisha bunifu zao katika kituo hicho, ili kuangalia namna zinavyoweza kuisaidia Serikali katika kuwahudumia wananchi.

Dkt. Jaha amesema hayo wakati akieleza umuhimu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), kushiriki katika Maadhimisho ya Kitaifa ya Elimu, Ujuzi na Ubunifu yaliyofanyika kitaifa jijini Tanga katika viwanja vya michezo vya Shule ya Sekondari ya Popatlal kuanzia Mei 25 hadi 31 mwaka huu.

“Maadhimisho haya yanaenda sambamba na lengo la kituo chetu cha eGOVRIDC la kuchochea ari kwa vijana wa Kitanzania kufanya utafiti na ubunifu wa TEHAMA ili kukuza na kujenga uchumi wa kidijitali”, alisema Dkt. Jaha.

Alibainisha kuwa, eGOVRIDC inafanya utafiti wa teknolojia zinazoibukia kama vile Sarafu ya Mtandaoni (Digital Currency), Block chain, Internet of Things (IOT) na Akili mnemba (Aritificial Intelligence), ili kuona ni namna gani teknolojia hizo zinaweza kutumika katika kubuni mifumo itakayoisadia Serikali katika utendaji kazi pamoja na kuwarahisishia wananchi kupata huduma. “Nitoe rai kwa vijana wa kitanzania kuleta bunifu za TEHAMA zinazohusiana na matumizi ya teknolojia mpya, ili kuweza kuzifanyia tafiti na kuona ni namna gani zitaweza kuongeza ufanisi katika utendaji kazi wa Serikali na kurahisisha upatikanaji wa huduma za Serikali kwa wananchi”, alisema Dkt. Jaha.

Baadhi ya washiriki waliotembelea banda la e-GA, walieleza kufurahishwa na huduma mbalimbali zinazotolewa na e-GA ikiwa ni pamoja na bunifu za mifumo mbalimbali ya TEHAMA na matumizi ya teknolojia mpya zinazoibuka.

Bw. Evance Sombe mmoja wa washiriki waliotembelea banda la e-GA alisema kuwa, amejifunza mengi kutoka e-GA ikiwemo utafiti na ubunifu kwenye teknolojia mpya ya Akili Mnemba (Artificial Intelligence) na mifumo mingine iliyosanifiwa na kutengezwa na Mamlaka kupitia Kituo chake cha Utafiti na Ubunifu.

“Nimejifunza matumizi ya teknolojia ya Akili Mnemba ‘Artificial Intelligence - AI’ inayolenga kujenga mifumo ya kompyuta inayoweza kufanya kazi kwa kufanana na akili ya binadamu, ni vizuri vijana kutembelea banda la e-GA, ili kuweza kujifunza mambo yanayohusu utafiti na ubunifu lakini pia kujikita katika masomo ya sayansi kwani fursa ni kubwa kwenye sekta ya TEHAMA” alisema Bw. Sombe.

Naye Bw. Hafidh Iddi mwanafunzi wa Kidato cha nne (4) katika Shule ya sekondari Mkwakani jijini Tanga, alisema amejifunza namna ambavyo e-GA imeweza kubuni na kutengeneza mifumo mbalimbali inayotumika Serikalini na namna wananchi wanavyoitumia kupata huduma za Serikali kidijitali.

> “Natumaini kuwa, mara baada ya kumaliza kidato cha sita (6) nitasomea fani ya TEHAMA ili kuweza kuisaidia Serikali kubuni mifumo itakayoongeza ufanisi katika utendaji kazi na hatimaye kutoa huduma bora na kwa wakati”
>
> Bw. Hafidh Iddi
>
> Mwanafunzi

Kutokana na mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia Bw. Hafidh alitoa rai kwa wanafunzi wenzake kusoma fani ya TEHAMA, ili kwenda sambamba na mabadiliko ya teknolojia na kuchochea ari ya ubunifu na utafiti katika maeneo mbalimbali ya teknolojia nchini.



# MFUMO WA MGov 2.0 WABORESHWA KUONGEZA UFANISI ZAIDI

Kutokana na maendeleo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika karne hii ya 21, matumizi ya simu za mkononi yameendelea kuongozeka ambapo kwa sasa simu zinatumika kwa matumizi mbalimbali na si kwa ajili ya mawasiliano pekee kama ilivyokuwa hapo awali.

Pamoja na kuongezeka kwa aina mbalimbali ya matumizi hayo, lakini pia simu imekuwa ni kifaa na kiungo muhimu kati ya Serikali na wananchi kwani, simu hutumiwa na Serikali kutoa huduma na kuwawezesha wananchi kupokea huduma hizo kidijitali kupitia simu ya mkononi mahali walipo.

Katika kuhakikisha wananchi wanapata huduma za Serikali kwa urahisi zaidi, Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) imetengeneza Mfumo wa Kutoa Huduma za Serikali kupitia Simu za Mkononi (mGov), wenye lengo la kuziwezesha taasisi za umma kuwahudumia wananchi kwa urahisi, uharaka, usalama na gharama nafuu kupitia simu zao za mkononi.

Aidha, mfumo huu umejumuisha huduma mbalimbali za Serikali na unatumia arafa (SMS) katika kutoa na kupokea taarifa ikiwemo SMS za ununuzi wa umeme (LUKU), SMS za huduma za malipo ya Serikali (GePG), huduma za kikodi (TRA), huduma za ardhi, huduma za afya (NHIF, CHF), huduma za kilimo, ajira, maji, elimu, sheria, haki, uwasilishaji wa maoni au mrejesho n.k.

Kutokana na mabadiliko ya teknolojia pamoja na maoni mbalimbali ya watumiaji wa mfumo wa m-GOV, e-GA iliamua kufanya maboresho katika mfumo huo kutoka mGov na kuwa mGov 2.0, kwa kuuongezea mfumo ufanisi zaidi katika utendaji kazi wake.

Kaimu Meneja wa Sehemu ya Huduma za Serikali kupitia Simu za Mkononi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Bw. Aziz Abdulaziz amesema kuwa, Mamlaka iliamua kufanya maboresho kwenye mfumo huo ili uweze kuendana na wakati na kuhimili mabadiliko ya teknolojia pamoja na kuwa bora zaidi katika usalama wake.

> "Awali Taasisi za Umma zilipokuwa zikihitaji kutengenezewa jina la mtumiaji (white listing of SenderID) ilizillazimu taasisi kutuma maombi yake e-GA na baada ya kupokelewa, yalitumwa kwa watoa huduma kwa ajili ya utekelezaji na kisha taasisi hizo zilitakiwa kufanya ufuatiliaji wa majibu ya ombi husika, ili kujua kama ombi limekamilika au bado, baada ya maboresho ya **mGov 2.0**, sasa taasisi inaweza kufuatilia utekelezaji wa ombi lake kupitia mfumo"
>
> Bw. Aziz Abdulaziz
> **Kaimu Meneja wa Sehemu ya Huduma za Serikali kupitia Simu za Mkononi**

Ameongeza kuwa, mfumo wa mGov 2.0 unaruhusu ujazaji wa dodoso kupitia simu za mkononi kwa njia ya sms, ambapo taasisi husika huandaa dodoso na kutuma kwa njia ya ujumbe mfupi (SMS) kwa wahusika, na ili mtu aweze kujaza dodoso hilo ni lazima ajiunge (subscribe), ndipo atatumiwa maswali yanayoambatana na majibu mbalimbali ambayo mjazaji wa dodoso atachagua jibu analodhani ni sahihi kwake, amefafanua Azizi.

Aidha, amebainisha kuwa, mfumo huu umewezeshwa na kuongezewa uwezo wa kuruhusu utumwaji wa ujumbe wa maandishi kwa ajili ya kujulisha jambo fulani kwa walengwa (notification sms).

"Kwenye mfumo wa mGov hapo awali mtu akiwa nje ya nchi alikuwa hawezi kupokea sms zinazotumwa kupitia mfumo, lakini baada ya kukamilika maboresho ya mGov 2.0 arafa (sms) zitaweza kutumwa nje ya nchi, na hii itasaidia sana kwa watu wanaofuatilia zabuni mbalimbali pamoja na mambo ya uwekezaji ambao wapo nje ya nchi," amesema Aziz.

Ameongeza kuwa, mfumo wa mGov 2.0 utaunganishwa na mfumo wa baruapepe Serikalini (GMS), ambapo utaziwezesha taasisi zinazoutumia mfumo huu ziweze kutuma baruapepe na ujumbe huo ukapokelewa kama ujumbe mfupi wa maandishi kwenye simu ya mkononi.

Akilezea faida za maboresho yaliyofan-




Afisa Habari Mwandamizi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Bi. Queenter Mawinda, akitoa elimu jinsi Mfumo wa huduma za Serikali kupitia simu mkononi yaani (MGOV) kwa mwananchi aliyetembelea banda la e-GA wakati wa maonyesho ya wiki ya Elimu, Ujuzi na Ubunifu

yika kwenye mfumo huo, Afisa TEHAMA sehemu ya Huduma za Serikali Kupitia Simu za Mkononi Bi. Erna Mwende, amesema kuwa usalama wa taarifa na takwimu zote umeimarika kwani teknolojia iliyotumika katika mGov 2.0 ni mpya na inaweza kutambua viashiria hatarishi vyote vya kiusalama.

Erna amesema kuwa, mGov 2.0 katika utendaji kazi wake imezigawanya moduli zake zilizopo kwenye mfumo (push sms, pull sms n.k), hivyo eneo moja linapokuwa na changamoto au linapokuwa katika hali ya kufanyiwa maboresho halitoathiri utendaji kazi wa moduli nyingine.

Amebainisha kuwa, awali upatikanaji wa ripoti uliilazimu taasisi husika kuwasiliana na e-GA ili kuweza kupata ripoti mbalimbali, lakini kwa sasa mfumo unatoa ripoti wenyewe na mtumiaji wa mfumo anaweza kupangilia kwenye mfumo atumiwe ripoti zipi na kwa njia gani kulingana na matakwa ya taasisi yake.

Aziz amesema kuwa, matarajio ya baadaye ni kuuwezesha mfumo huo uwe rafiki zaidi ili kila Tasisi ya Umma iweze kujihudumia yenyewe ndani ya mfumo bila kuhitaji msaada wa mtu mwingine ili kuepusha mianya inayoweza kuleta urasimu.

Mfumo wa mGov 2.0 umeunganishwa na watoa huduma wote wa simu za mkononi nchini Tanzania ambao ni TTCL, Airtel, Vodacom, Tigo/Zantel na Halotel, mfumo unatoa huduma za ujumbe mfupi wa maandishi (SMS) kupitia namba jumuishi 15200 na 15201 pamoja na huduma za menyu ya USSD kupitia namba jumuishi *152*00#, na unaziruhusu Taasisi za Umma kutoa huduma kupitia namba binafsi za taasisi, kama vile *113# ya PCCB inayotoa huduma ya kuripoti matukio ya rushwa.


**“Kwasasa tupo katika hatua za mwisho za kuwezesha matumizi ya mwitiko wa sauti (Interactive Voice Response) ambapo taasisi zinazotumia mfumo huu, zitakuwa na uwezo wa kuwafikishia huduma wananchi kwa njia ya sauti ambapo itakuwa msaada mkubwa kwa watu wenye changamoto ya kuona pamoja na wale wasiojua kusoma”**

Bw. Aziz Abdulaziz

Kaimu Meneja wa Sehemu ya Huduma za Serikali kupitia Simu za Mkononi.



# MANISPAA YA TABORA YAOKOA ZAIDI YA MILIONI 160 KILA MWAKA KUPITIA MFUMO WA e-BOARD




**"Mfumo wa e-Board umetusaidia kukoa fedha nyingi tulizokuwa tukitumia kuwalipa waendesha vikao kwaajili ya kusambaza makabrasha kwa madiwani pamoja na ununuzi wa vifaa mbalimbali vilivyokuwa vikitumika katika uandishi wa vikao kila mwaka"**

**Bw. Elias Mahwago Kayandabila**
Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Tabora

Matumizi ya mfumo wa kuwezesha uratibu wa shughuli za uandaaji wa vikao mbalimbali vya bodi na menejimenti katika halmashauri na Taasisi za Umma (e-Board), yameiwezesha Halmashauri ya Manispaa ya Tabora kuokoa zaidi ya shilingi milioni 160, zilizokuwa zikitumika katika ununuzi wa vifaa mbalimbali vya uchapishaji na uaandaaji wa muhtasari wa vikao kila mwaka.

Hayo yamebainishwa hivi karibuni na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa hiyo Bw. Elias Mahwago Kayandabila, ofisini kwake mjini Tabora wakati akieleza faida walizozipata mara baada ya kuanza kutumia mfumo huo.

Alieleza kuwa, Manispaa ya Tabora imeanza kutumia mfumo wa e-Board Julai 2023, na tangu wakati huo imepata faida nyingi ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa ufanisi wa uendeshaji wa vikao na kuokoa gharama, kwani kila mwaka Manispaa hiyo ilikuwa ikitumia zaidi ya shilingi Milioni 160 kwa ajili ya kulipa makarani pamoja na ununuzi wa vifaa mbaimbali.

Aidha, Kayandabila alitoa rai kwa halmashauri zote nchi ambazo hazijaanza kutumia mfumo wa e-Board katika uendeshaji wa shughui zao zianze kutumia mfumo, huo kwani utawasaidia katika kuongeza ufanisi na kuokoa gharama za uendeshaji wa vikao.

''Sisi tulianza kutumia mfumo wa e-Board ili kuendana na kasi ya mabadiliko ya Teknolojia na kwakweli tumeona manufaa makubwa sana, ukilinganisha hapo awali, hivyo niziombe halmshauri nyingine zisiogope kuingia kwenye matumizi ya TEHAMA kwani hawatajutia'', alisistiza Bw. Kayandabila.

Kwa upande wake Mstahiki Meya wa Manispaa hiyo Mhe Ramadhani Shabani Kapela, alisema kwa kutumia mfumo wa e-Board mpaka sasa wamekwishafanya vikao tisa (9) vya kamati ya fedha, vikao 32 vya kamati za kawaida, vikao viwili (02) na mabaraza ya madiwani matatu (3) na kwa kipindi chote hicho hawajawahi kupata changamoto yoyote katika mfumo.

''Matumizi ya mfumo huu ni jambo la kujivunia sana kama Manispaa, sisi tumekuwa tukiutumia mfumo huu karibu mwaka mzima sasa, mwanzo madiwani walipata tabu kidogo kulingana na ugeni wa matumizi ya vishikwambi, lakini kwa sasa kila mmoja anaufurahia kwani hatujawahi kupata changamoto yoyote''Alisema

Naye Hussein Masoud Luziga ambaye ni mwandishi wa vikao na mikutano katika Manispaaa ya Tabora alisema, hapo awali walikuwa wakipata usumbufu mkubwa katika uandaaji wa muhtasari na usambazaji wa taarifa za kikao, lakini mara baada ya kuanza kutumia mfumo wa e-Board, wamekuwa wakiweka taarifa zote ndani ya mfumo hivyo umeondoa usumbufu wa kuzunguka kusambaza makabrasha kwa madiwani na wajumbe wa vikao vya Bodi

Kwa upande wake Diwani wa kata ya Ikomwa manispaa ya Tabora Mhe. Salum Magembe alisema, mfumo wa e-Board umemuwezesha kuhudhiria vikao vya Baraza hata kama yuko nje ya Manispaa, huku Diwani wa viti maalumu katika Manispaa hiyo Mhe. Marry Bisambi akiipongeza e-GA kwa kubuni mfumo huo ambao wao kama madiwani wa halmshauri ya Tabora wamepokea vizuri kutokana na wingi wa faida zake.

Mfumo wa e-Board ni mfumo uliotengenezwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) kwa ajii ya kuwezesha uratibu wa shughuli za uandaaji wa vikao mbalimbali vya Bodi na Menejimenti katika Halmashauri na Taasisi za umma



**Bw. Elias Mahwago Kayandabila**
Mkurugenzi wa Halmashauri Manispaa ya Tabora




# GISP YASAIDIA KUONGEZA UFANISI WA MIRADI YA TEHAMA SERIKALINI

Uwasilishaji wa miradi ya TEHAMA Serikalini katika Tovuti ya Huduma za TEHAMA Serikalini (GISP), umetajwa kuongeza ufanisi wa miradi hiyo kutokana na kutolewa ushauri wa kitaalamu katika hatua za awali unaofanywa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), kabla ya utekelezaji wa miradi hiyo.

Kauli hiyo imetolewa hivi karibuni na Meneja wa Usimamizi wa Miradi ya TEHAMA kutoka Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Bw.Godfrey Masanja, wakati alipofanya mahojiano malum kwa njia ya simu na mwandishi wetu kuhusu umuhimu wa mfumo wa GISP katika kuongeza tija na ufanisi wa miradi ya TEHAMA Serikalini.

“Kwa mujibu wa kifungu Na. 24 cha Sheria ya Serikali Mtandao Na. 10 ya Mwaka 2019, Taasisi za Umma zinazokusudia kutekeleza miradi ya TEHAMA zinapaswa kuwasilisha taarifa za miradi hiyo kwa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA)kupitia Mfumo wa GISP, ili kupata kibali kabla ya kuanza kutekeleza miradi hiyo”, alisema Bw. Masanja.

Alifafanua kuwa, mfumo wa GISP una lengo la kuharakisha na kupunguza muda uliohitajika kuwasilisha maombi ya huduma kwa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), ukilinganisha na njia nyingine kama vile barua.

Alibainisha kuwa, mfumo huo umesaidia kuongeza ufanisi katika utendaji kazi wa Serikali kwani unarahisisha ufuatiliaji na upatikanaji wa mrejesho wa hatua za utekelezaji wa maombi ya huduma za TEHAMA yaliyowasilishwa na Taasisi za Umma kwa Mamlaka ya Serikali Mtandao

“Mfumo wa GISP umesaidia kurahisisha mchakato wa utoaji wa huduma za TEHAMA kwa kupunguza wingi wa taarifa, hatua na muda unaohitajika kuwasilisha na kupata huduma za TEHAMA” alisema Bw. Masanja

Aidha, Bw. Masanja alifafanua kuwa taarifa zinazowasilishwa kupitia mfumo wa GISP ni pamoja na andiko la mradi (Project Concept Note/Proposal) lililoidhinishwa na Kamati ya Usimamizi wa TEHAMA ya Taasisi (Institutional ICT Steering Committee), ambapo Mamlaka hufanya mapitio ya andiko la mradi huo lililoidhinishwa na kutoa kibali cha mradi huo ndani ya siku 14 tangu kuwasilishwa kwa taarifa za mradi.

Aliongeza kuwa, uwasilishwaji wa taarifa za miradi kwenye mfumo wa GISP umesaidia kupunguza urudufu wa jitihada kwa kuepuka ujenzi wa mifumo inayofanya kazi zinazofanana na hivyo kupunguza matumizi ya fedha yasiyo ya lazima katika utekelezaji wa miradi.

“e-GA inapokea na kupitia taarifa zote za miradi zinazowasilishwa na Taasisi za Umma, na kisha kutoa idhini au maelekezo mbadala ili kuondoa uwezekano wa urudufu wa jitihada na kuepuka matumizi ya fedha yasiyo ya lazima”, alisisitiza Bw. Masanja.

Sambamba na hilo Bw. Masanja aliongezea kuwa, mfumo wa GISP umesaidia kuimarisha usalama wa mifumo ya TEHAMA Serikalini kwa kuzingatia matumizi ya teknolojia zinazoendana na mazingira ya sasa, na kuhakikisha mifumo inayopatikana baada ya utekelezaji wa miradi husika inakuwa na uwezo wa kubadilishana taarifa na mifumo mingine ya TEHAMA Serikalini.

Pia, Mfumo wa GISP umeiwezesha na kuipatia nafasi e-GA ya kutambua miradi ya TEHAMA inayokusudiwa au inayotekelezwa na Serikali, na kuweza kutoa ushauri wa kitaalam kwa wakati kwa watekelezaji wa miradi hiyo, alifafanua Bw. Masanja.

Naye Meneja wa Huduma za Sheria e-GA ASP Raphael Rutaihiwa alisema kuwa, kwa mujibu wa Sheria ya Serikali Mtandao Kifungu Na. 57 kinaielekeza e-GA kuchukua hatua stahiki kwa taasisi ambayo itakiuka taratibu za kuwasilisha taarifa za miradi ya TEHAMA kwenye mfumo, kwani kunainyima nafasi Mamlaka kushauri kwa wakati kuhusu utekelezaji wa miradi hiyo.

Bw. Rutaihiwa amezitaka Taasisi za Umma kuzingatia Sheria ya Serikali Mtandao kwa kuwasilisha taarifa za miradi ya TEHAMA kupitia GISP, kwa miradi yote inayotekelezwa na iliyokwisha kutekelezwa, pamoja na miradi yote ya TEHAMA inayokusudiwa kutekelezwa.

Akizungumzia taratibu za uwasilishwaji wa miradi kwenye mfumo huo, Bw. Masanja alisema Taasisi za Umma zinatakiwa kuandika barua kwenda Mamlaka ya Serikali Mtandao, kuomba kusajiliwa katika mfumo wa GISP ikiwa na taarifa za taasisi na wataalam wa TEHAMA wa taasisi hiyo wanaokusudiwa kufunguliwa akaunti katika mfumo wa GISP (majina, barua pepe na namba ya simu).

Aidha, Taasisi zilizowasilisha taarifa za miradi kwenye GISP na kupewa kibali cha kuendelea na utekelezaji wa miradi hiyo, zinatkiwa kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa miradi hiyo kupitia GISP ili kuwa na taarifa sahihi za utekelezaji wa mradi, pamoja na kusaidia utoaji wa ushauri wa kitaalam kulingana na hali halisi ya utekelezaji wa miradi hiyo kwa vipindi husika, alisema Bw. Masanja.

Taasisi zinaweza kuwasiliana na dawati la msaada wa kiufundi la Mamlaka ya Serikali Mtandao kupitia barua pepe: **egov.helpdesk@ega.go.tz** au simu: **0764292299 au 0763292299** kwa msaada zaidi. Aidha, mfumo wa GISP unapatikana kupitia **https://gisp.gov.go.tz.**

# WAKAGUZI WA NDANI WA SERIKALI WATAKIWA KUELIMISHA KUHUSU MAENDELEO YA TEHAMA



Wakaguzi wa ndani kutoka katika Taasisi mbalimbali za umma wakiwa katika mafunzo ya Sheria, kanuni, viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao Jijini Arusha

WAKAGUZI wa Ndani wa Serikali, wametakiwa kujifunza na kupata maarifa mapya ili kuendana na mabadiliko ya Teknolojia ya Habari na mawasiliano (TEHAMA) yanayojitokeza katika maeneo yao ya kazi.

Wito huo umetolewa na Meneja wa Huduma za Sheria wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi (SACP) Raphael Rutahiwa, wakati wa kufunga mafunzo ya siku nne ya kuwajengea uwezo Wakaguzi wa Ndani wa Serikali juu ya namna ya kukagua mifumo ya TEHAMA katika taasisi zao.

Mafunzo hayo ya Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao kwa Wakaguzi wa Ndani wa taasisi za umma, yaliratibiwa na e-GA pamoja na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali (IAG), yalifanyika jijini Arusha kuanzia April 22 hadi 25 mwaka huu.

Lengo la mafunzo hayo ni kuhakikisha Wakaguzi wa Ndani wa Serikali wanasimamia kwa weledi na kuhakikisha taasisi zao zinazingatia na kutekeleza Sheria, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao katika miradi yote ya TEHAMA.
Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao, SACP Rutahiwa alisema, kada ya ukaguzi ina nafasi kubwa na ni chachu katika wakati huu wa mageuzi ya kidigiti nchini.

> **“Mageuzi ya kidigiti ni vita, hivyo tunahitaji mbinu ili kushinda vita hii na moja ya silaha ni kusoma au kujisomea, kwakuwa Serikali yetu imeshaamua kuingia na haitorudi nyuma katika matumizi ya TEHAMA ni lazima tujiandae kushiriki katika mageuzi haya kwa kupata maarifa mapya”**
>
> SACP Raphael Rutahiwa.
> Meneja Huduma za Sheria - eGA

Aliongeza kuwa, kada ya ukaguzi ina wajibu mkubwa katika kuhakikisha Serikali inapata thamani ya uwekezaji katika mifumo na miundombinu ya TEHAMA.

Kwa upande wake Mkaguzi wa Ndani Mwandamizi kutoka Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali (IAG) Bi.Donisia Tesha, aliwataka Wakaguzi wa Ndani kuzingatia maarifa waliyoyapata katika mafunzo hayo, ili kuhakikisha miradi ya TEHAMA Serikalini inaleta tija.



SACP Raphael Rutahiwa,
Meneja Huduma za Sheria e-GA.



**Bi. Ummy Mohammed Wayayu**
Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela

# MANISPAA YA ILEMELA YATAJA FAIDA ZA KUTUMIA MFUMO WA e-BOARD

Matumizi ya Mfumo wa kuwezesha uratibu wa shughuli za uandaaji wa vikao mbalimbali vya bodi na menejimenti katika Halmashauri na Taasisi za Umma. (e-Board), umetajwa kurahisisha uendeshaji wa vikao na kupunguza gharama za maandalizi katika halmashauri ya Manispaa ya Ilemela jijini Mwanza.

Akizungumza kuhusu mfumo huo ofisini kwake jijini Mwanza, Mkurugenzi wa halmashauri ya Manispaa ya Ilemela Bi. Ummy Mohammed Wayayu, amesema kuwa kabla ya halmashauri hiyo kuanza kutumia mfumo wa e-Board mwaka 2023, fedha nyingi zilikuwa zikitengwa katika ununuzi wa shajara, wino na vifaa vingine kwa ajili ya vikao vya Madiwani na Menejimenti.

"Kwa mwaka tulikuwa tunatumia takribani shilingi milioni 200 hadi 300 katika maandalizi ya uendeshaji wa vikao, lakini kwa sasa gharama hizo hatuna tena kwakuwa tunatumia mfumo huu wa e-Board, ambao umetusaidie kupeleka fedha hizo katika mambo mengine ya muhimu katika halmashauri," alisema Bi.Ummy.

Aliongeza kuwa, mfumo wa e-Board umesaidia kupunguza gharama za kudurufu taarifa mbalimbali na badala yake zinapakiwa kwenye mfumo na madiwani wanapakuwa na kuendelea kuzifanyia kazi.

Licha ya mfumo huo kusaidia katika kupunguza gharama, Mkurugenzi huyo alisema kwamba mfumo wa e-Board umesaidia katika upigaji wa kura za siri katika uchaguzi wa Wenyeviti wa Kamati pamoja na uchaguzi wa Mstahiki Meya.

"Hapo awali usiri katika chaguzi hizo ulikuwa mdogo sana, lakini kwa sasa tunatumia mfumo hivyo kura zinakuwa za siri na kila mtu ndani ya nafsi anajua amemchagua nani," alifafanua.

Aidha, Bi Ummy aliongeza kuwa, mfumo wa e-Board unawasaidia madiwani kushiriki katika kila kikao hata wanapokuwa nje ya halmashauri hiyo kwa kutumia vishkwambi ambavyo vimewezeshwa matumizi ya mfumo huo na kugawiwa kwa kila diwani.

Kwa upande wake Mstahiki Meya wa Halmashauri hiyo Mheshimiwa Renatus Mulunga, alisema kuwa mfumo wa e-Board umewasaidia madiwani kuendesha vikao vyao kwa ufanisi ili kuboresha huduma za wananchi wa Ilemela.

"Nina miaka 25 kwenye udiwani, huko nyuma ilikuwa lazima ujaze gari mafuta kwa ajili ya kusambaza makarabrasha, lakini kupitia mfumo wa e-Board kila diwani anapata taarifa na makabrasha yake popote alipo kupitia mfumo na kuanza kuyafanyia kazi," alisema Bw. Mulunga.

Mhe. Mulunga alitoa rai kwa halmashauri nyingine ambazo bado hazijaanza kutumia mfumo wa e-Board, kufanya ziara halmashauri ya Manispaa ya ilemela au kuwasiliana na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), ili zipate uelewa kuhusu mfumo huo.

Naye Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA wa Halmashauri ya Ilemela Bw.Isaack Tanguye, alisema kwamba halmashauri hiyo ilianza kutumia mfumo wa e-Board baada ya kupata malalamiko kuhusu gharama kubwa za uandaaji wa vikao.

Alisema kwamba baada ya malalamiko hayo kuwa mengi, kitengo chake kiliamua kuwasiliana na e-GA kuomba mfumo wa e-Board, na baadaye walianza kuwajengea uwezo Madiwani pamoja na Menejimenti ya halmashauri hiyo ili kuanza kufanya vikao vyao kidijiti.

Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela ndiyo halmashauri ya kwanza kuanza kutumia mfumo huu wa e-board kati ya halmashauri 184 nchini, mfumo huu umesanifiwa na kutengenezwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA).

# KUTOKA KITUO CHA UTAFITI, UBUNIFU NA UENDELEZAJI WA SERIKALI MTANDAO



# 'TWIGA CLOUD' MKOMBOZI WA FAILI ZAKO ZA KIDIGITI

Watu wengi hupoteza mafaili yao muhimu mara tu simu au kompyuta zao zinapoharibika au kupotea, huenda hata wewe ukawa ni miongoni mwa waathirika hao.

Habari njema ni kuwa mwarobaini wa tatizo hili umepatikana, na sasa mafaili yako yatakuwa salama hata kama utapoteza simu au kompyuta yako kuharibika.


Naam! Ni kupitia mfumo wa kuhifadhi mafaili yako mkondoni wa 'Twiga Cloud' unaweza kutunza mafaili yako wakati wowote na kuwa na uhakika wa usalama wake hata kama kifaa chako (kompyuta, simu janja, kishwambi n.k), ulichotumia kuandaa na kuhifadhi mafaili yako kitapotea au kuharibika.

Mfumo huu una moduli tatu 'Twiga Drive, Twiga Archive na Twiga Collabora' ambazo zote zinamuwezesha mtumiaji kufanya kazi za kuhifadhi, kutunza na kuhariri mafaili yake kwa usalama na wepesi zaidi mtandaoni.

Kupitia moduli yake ya 'Twiga drive', unaweza kuhifadhi picha na nyaraka zako muhimu kama vile vyeti vya kitaaluma, hati za nyumba na mashamba, video za kumbukumbu ya matukio muhimu ulizohifadhi kwenye simu yako au ulizohifadhi katika komputa yako sawa na mifumo ya kigeni kama vile 'Google Drive' na 'Drop Box'.

Licha ya kuwa na uwezo wa kutunza mafaili yako kidigiti, mfumo huu una upekee zaidi kwakuwa na moduli ya 'Collabora' ambayo inafanya kazi kama 'Google docs', kupitia moduli hii ya 'Collabora' iliyomo katika mfumo huu, unaweza kuandika andiko lako na ukawatumia watu wengine na mkaweza kuhariri kwa pamoja, moduli hii imesanifiwa kuwezesha wananchi ikiwemo waandishi wa tafiti, waandishi wa habari na maandiko mengine ambayo yanahitaji mapitio ya mtu zaidi ya mmoja.

Kwenye 'Collabora' kila kitu kimekuwa rahisi sana, unaweza ukaandika andiko lako pale na ukalituma kwa watu wengine na wote wakaweza kulifanyia kazi kwa wakati mmoja iwe kwenye kuhariri au kuongezea taarifa kwenye andiko husika.




Moduli ya tatu katika mfumo huu ni 'Twiga Archive', module hii inamuwezesha mtumiaji kutunza nyaraka zake kidijiti, katika moduli hii nyaraka zote zitatumwa kupitia teknolojia ya Akili Mnemba na 'Machine Learning', kwa kutumia teknolojia hiyo, nyaraka na mafaili yote yatachakatwa na kupangwa kwa ustadi zaidi kwa kuweka lebo na mpangilio (indexing and tagging) ili kumrahishia mtumiaji asipoteze muda wakati analihitaji kulifanyia kazi.

Vilevile, moduli hii imesanifiwa na teknolojia ya 'Optical character recognition - OCR' ambayo inamsaidia mtumiaji kutafuta faili lake kwenye mfumo kwa kutumia neno lolote analolikumbuka lililomo kwenye andiko lake, kwa sasa moduli hii ya Twiga Archive itatumika kwa taasisi na mashirika ya umma pekee.


Mfumo huu tayari upo hewani na mwananchi yeyote anaweza kuutumia, endapo utajisajili katika mfumo huu, utapata nafasi ya GB 1 kwenye Twiga Drive ili uweze kuhifadhi mafaili yako, kwa upande wa taasisi au kampuni itapewa GB 5 za bure kwa ajili ya kutunza taarifa/nyaraka zake.

Vilevile mfumo huu umezingatia usalama, unyeti wa taarifa na unapatikana muda wote kwa mtu yeyote ambaye amejisajili.

Mfumo unapatikana kupitia simu janja au kompyuta kwa kupakua aplikesheni tumizi kwenye playstore (Android), Appstore (iOS) au Microsoft (Windows) kwa kutafuta (search) 'Twiga Cloud' ambako kwa sasa utapata kipengele kimoja tu cha Twiga drive.

Pia, unaweza kuvinjari kupitia (web browser) kwa kutumia anuani 'https://twigacloud.tz' kujisajili na kufurahia ubunifu huu wa kitanzania kwa kupata vipengele vya twiga drive na collabora.

Mfumo wa Twiga Cloud, umesanifiwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), kupitia Kituo chake cha Utafiti, Ubunifu na Uendelezaji wa Serikali Mtandao (e-GOVRIDC).




# e-GA NA MKAKATI WA KUIBUA NA KUKUZA VIPAJI KWA VIJANA WAZAWA KATIKA ENEO LA TEHAMA

"Uadilifu na ubunifu kwa utoaji wa huduma bora kwa umma" huu ndio moto wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), unaoangaza njia inayochochea bunifu mbalimbali za TEHAMA zitakazosaidia kuboresha utoaji wa huduma za Serikali kidijitali.

Ili kufikia mafanikio haya, Oktoba 2019 e-GA ilianzisha Kituo cha Utafiti, Ubunifu na Uendelezaji wa Serikali Mtandao (eGOVRIDC), kwa lengo la kuimarisha na kukuza tafiti pamoja na bunifu za TEHAMA, kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa sekta hiyo.

Miongoni mwa wadau hao ni Taasisi za Vyuo Vikuu ambapo, hadi sasa e-GA imeingia Mkataba wa Makubaliano (MOU) na Taasisi 14 za Vyuo vikuu nchini zinazotoa mafunzo ya TEHAMA kwa ngazi mbalimbali.

Taasisi hizo ni pamoja na Chuo Kikuu Dodoma (UDOM), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Chuo Kikuu Mzumbe, Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM), Chuo cha Teknolojia cha Dar es Salaam (DIT), Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) n.k.

Aidha, malengo ya makubaliano hayo ni pamoja na kuratibu shughuli za utafiti wa Serikali Mtandao kwa kuweka mazingira wezeshi ya tafiti hizo, kuhimiza ubunifu kwa vijana wazawa katika eneo la TEHAMA, kupunguza utegemezi wa wakandarasi wa nje na kutengeneza mifumo ya TEHAMA iliyo salama zaidi (salama dhidi ya matishio ya kimtandao).

Kupitia kituo hiki, vijana mbalimbali wa kitanzania wanaosoma fani ya TEHAMA katika Vyuo hivyo, wamepata fursa ya kujifunza kwa vitendo na hatimaye kuibua na kukuza vipaji vyao katika eneo la uvumbuzi wa mifumo mbalimbali ya TEHAMA, itakayosaidia kutatua changamoto za kiutendaji Serikalini na kuimarisha utoaji wa huduma kwa wananchi.

Meneja wa Huduma za Sheria Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi (SACP) Rafael Rutahiwa anasema kuwa, makubaliano ya ushirikiano kati ya e-GA na Vyuo Vikuu yamesaidia kuziba pengo kati ya wahitimu wa Vyuo Vikuu na ujuzi unaohitajika katika soko la ajira.

Anabainisha kuwa, ushirikiano huo umesaidia Vyuo Vikuu nchini kubaini maeneo yanayotakiwa kuboreshwa katika mitaala ya kufundishia ili kutengeneza vijana wanaoendana na soko la ajira.

"Vilevile, ushirikiano wetu na Vyuo Vikuu umesaidia kutoa nafasi kwa vijana wa Vyuo hivyo kujifunza kwa vitendo na kuweza kushindana katika soko la ajira ndani na nje ya nchi, pamoja na kuwawezesha kujiajiri wenyewe kwakuwa tayari wanakuwa na ujuzi unaohitajika sokoni", anasisitiza SACP Rutahiwa.

Sambamba na hilo, SACP Rutahiwa anabainisha kuwa mafunzo yanayotolewa kwa vijana hao yamekuwa yakihusisha matumizi ya teknolojia huria 'open source' katika utengenezaji wa mifumo rahisi ambayo inaweza kutumiwa na Serikali na hivyo kuondoa urudufu wa mifumo.

"Pamoja na utoaji wa fursa ya mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi wa Vyuo Vikuu, pia tunashirikiana na vyuo hivyo katika tafiti mbalimbali kwenye eneo la TEHAMA ambazo zinalenga kuimarisha Serikali Mtandao", anasema Rutaihiwa.

Aidha, Rutahiwa anabainisha kwamba kupitia eGOVRIDC, Serikali imeweza kuondokana na utegemezi wa utengenezaji wa mifumo ya TEHAMA kwa kutumia wakandarasi wa kigeni ambao hapo awali walitengeneza mifumo hiyo kwa gharama kubwa, huku baadhi yao wakishindwa kutengeneza mifumo kulingana na taratibu za kiutendaji ndani ya taasisi, na hivyo mifumo hiyo kushindwa kutatua matatizo ya taasisi husika na kusababisha urudufu wa mifumo.

> **"Kituo chetu cha utafiti na ubunifu kinabuni na kutengeneza mifumo mbalimbali ya TEHAMA inayoweza kutumika Serikalini na kutatua changamoto zilizopo, tunahakikisha kabla ya utengenezaji tunafahamu taratibu za utendaji wa taasisi husika na mwisho kabisa ni lazima mifumo hiyo itatue changamoto zilizokuwepo"**
>
> **SACP Rafael Rutahiwa.**
> Meneja wa Huduma za Sheria e-GA







Ametaja baadhi ya mifumo iliyobuniwa na kutengenezwa na kituo hicho, ambayo inatumiwa na taasisi mbalimbali za umma ni pamoja na mfumo wa uendeshaji vikao wa e-Mikutano, mfumo wa uandandaaji na uendeshaji wa vikao vya Menejimenti na Halmashauri wa e-Board pamoja na mfumo wa kutuma na kupokea maoni au pongezi Serikalini wa e-Mrejesho.

"Ushirikiano wetu sisi e-GA na Vyuo Vikuu umeleta matokeo chanya na mazuri, na sisi e-GA tutandelea kuimarisha ushirikiano huu ili kukuza ujuzi na vipaji kwa vijana wa Kitanzania wabunifu katika TEHAMA na hatimaye tuweze kujenga kizazi chenye umahiri katika dijitali", anasema Rutahiwa.

Kwa upande wake Meneja wa Kituo cha Utafiti, Ubunifu na Uendelezaji wa Serikali Mtandao (eGovRIDC) Dkt. Jaha Mvulla, anasema lengo kubwa la kituo hiki ni kufanya utafiti na ubunifu kwenye eneo la TEHAMA, kuibua teknolojia zitakazosaidia Serikali katika utendaji kazi lakini pia kukuza na kuendeleza vijana wabunifu kutoka vyuoni.

Anabainisha kuwa, e-GA inawapa fursa wanafunzi wa kada ya TEHAMA kupata picha halisi ya masomo wanayoyasoma pamoja na hali halisi ya sekta husika ilivyo katika soko shindani la ajira, kwa kuwajengea uwezo wanafunzi na kuchochea ubunifu na vipaji vyao.

"Programu mbalimbali zinazoendeshwa na kituo hiki zimewasaidia wanafunzi wengi wa vyuo vikuu, kuongeza ujuzi na uzoefu katika kuzielewa teknolojia mpya ili kuchochea maendeleo na mageuzi makubwa ya Serikali ya kidigitali, kutatua changamoto za kiteknolojia na kubuni mifumo ya TEHAMA inayoweza kutumika Serikalini kwa lengo la kuongeza ufanisi wa utendaji kazi", anasisitiza Dkt. Jaha na kuongeza kuwa,

"e-GA inajivunia uvumbuzi wa mfumo tumizi wa e-Mrejesho ambao tayari umetambuliwa na Benki ya Dunia (WB) pamoja na Umoja wa Mataifa (UN) kama mfumo bora unaotoa ushirikishaji kwa wananchi kwakuwa wananchi wanaweza kutuma maoni, malalamiko au pongezi kwenda kwenye taasisi za umma pamoja na kufuatilia utekelezaji wake".

Mfumo mwingine unaotokana na zao la kituo chetu cha eGOVRIDC ni mfumo wa kuwezesha uratibu wa shughuli za uandaaji wa vikao mbalimbali vya bodi na menejimenti, ujulikanao kama e-Board, ambao hadi sasa taasisi zaidi ya 60 zinatumia mfumo huu, zikiwemo Wizara, Taasisi na Halmashauri mbalimbali.

"Tunajivunia kuona vijana wengi waliopata mafunzo kutoka hapa eGOVRIDC, wamekuwa mahiri katika maeneo mbalimbali ya teknolojia na kupata fursa za ajira ndani na nje ya nchi, hii inadhihirisha kuwa, Mamlaka imewasaidia na kuwajengea uwezo mkubwa vijana hawa wa kuweza kushindana katika soko la ajira duniani", anasema Dkt. Jaha.

Pamoja na mafanikio hayo yaliyopatikana kupitia kituo hiki, e-GA imeandaa mpango endelevu wa kutatua changamoto zilizopo kupitia tafiti na bunifu mbalimbali kwenye matumizi ya teknolojia mpya zinazochipukia 'Emerging Technologies' na kujivunia baadhi ya mifumo iliyotengenezwa kupitia teknolojia hizo ikiwemo Internet of Things (IOT), Blockchain, Machine Learning na Artificial Intelligence (AI).

"e-GA itaendelea kuboresha miundombinu ya kituo na mazingira yake ikiwemo kuongeza vifaa tumizi kwa ajili ya kuwezesha mafunzo kwa vitendo kufanyika kwa ukamilifu, ili kukiwezesha kituo hiki kiendelee kufanya kazi zake za utafiti na ubunifu kwa ufanisi zaidi", anasema Dkt. Jaha.

Mmoja wa washiriki wa programu maalumu ya mafunzo kazini 'Internship' inayoendeshwa na kituo hiki Bw. Claud Charles, ameishukuru e-GA kwa kutoa fursa ya mafunzo hayo yaliyomsaidia kutengeneza moja ya mfumo utakaoisaidia Serikali katika utendaji kazi wake.

"Naishukuru sana e-GA kwa kunipa nafasi hii kwani kwa kushirikiana na watumishi wake tuliweza kutengeneza mfumo wa Webguard utakaosaidia kufuatilia ufanisi wa mifumo mingine ya Serikali ikiwemo tovuti za Serikali na kubaini kama zipo sawa au la", anasema Bw. Claud.

Aidha, Bw. Claud ameiomba e-GA kuendeleza ushirikiano uliopo na Vyuo Vikuu nchini katika shughuli mbalimbali za utafiti na ubunifu ili kuibua vijana wenye vipaji katika TEHAMA.

Naye Bi. Miriam Shaka, ambaye pia ni mshiriki wa program hiyo anabainisha kwamba anatarajia kuona mafunzo wanayoendelea kuyapata yanawasaidia kuzielewa teknolojia mpya, na kutumia teknolojia hizo katika uvumbuzi wa mifumo mbalimbali itakayosaidia Serikali katika utendaji wa kazi.

"Nafasi hii tuliyopata ni muhimu sana kwetu lakini pia kwa manufaa ya taifa letu, hivyo tutaitumia kujifunza na kupata ujuzi utakaosaidia kuleta maendeleo kwa taifa letu sambamba na kukuza uchumi wetu", anasisitiza Miriam.

Hadi sasa takribani vijana 300 wamepata fursa na kunufaika na programu inayoendeshwa katika kituo hiki, huku matarajio ya e-GA yakiwa ni kujenga kituo kikubwa cha utafiti na ubunifu kitakachoweza kuchukua wanafunzi wengi zaidi wa mafunzo kwa vitendo kwa mara moja.

# MATUKIO KATIKA PICHA

## SERIKALI INATHAMINI MCHANGO WENU KATIKA USANIFU NA UJENZI WA MFUMO WA e-WATUMISHI : WAZIRI MKUU





Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa (Mb), akimkabidhi tuzo ya heshima Afisa TEHAMA Mwandamizi wa e-GA Bw. Shukuru Kawago.



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa (Mb), akimkabidhi tuzo ya heshima Afisa TEHAMA wa e-GA Bw. Dislaus Mahenge.



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa (Mb), akimkabidhi tuzo ya heshima Afisa TEHAMA Mwandamizi wa e-GA Bw. Christian Hebert .



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa (Mb), akimkabidhi tuzo ya heshima Afisa TEHAMA Mwandamizi wa e-GA Bw. Jamili Rajabu Chewe.

# WIKI YA UTUMISHI WA UMMA


## 16 - 23, Juni 2024



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora **Mhe. George B. Simbachawene (Mb),** akisaini kitabu cha wageni alipotembelea banda la Mammlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), wakati wa maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yaliyofanyika katika viwanja vya chinangali Park Jijini Dodoma.




Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora **Mhe. George B. Simbachawene (Mb),** akisikiliza maelezo kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa e-GA Mhandisi Benedict Ndomba wakati alipotembelea banda la e-GA.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora **Mhe. George B. Simbachawene (Mb),** akisikiliza maelezo kutoka kwa Afisa TEHAMA wa e-GA Bi. Khadija Mzenzi wakati alipotembelea banda la e-GA.

# SHUKRANI KWA UDHAMINI




Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mhe. Kassim Majaliwa (Mb),** akikabidhi cheti cha shukrani ya udhamini kwa Afisa Habari Mwandamizi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Bi. Queenter Mawinda, e-GA ni miongoni mwa wadhamini katika Maadhimisho ya Kitaifa ya Elimu, Ujuzi na Ubunifu yaliyofanyika mwezi Mei mwaka huu jijini Tanga.




Afisa Habari Mwandamizi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Bi. Queenter Mawinda, baada ya kupokea cheti cha udhamini katika maadhimisho ya kitaifa ya Elimu, Ujuzi na Ubunifu.

# MAADHIMISHO YA KITAIFA YA ELIMU, UJUZI NA UBUNIFU.

## 25 - 31, Mei 2024




Mkuu wa Mkoa wa Tanga **Mh. Balozi Dkt. Batilda S. Buriani** (wa pili kulia), akisikiliza maelezo kuhusu huduma za Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) kutoka kwa Afisa TEHAMA wa Mamlaka Bw. Tumaini Masinsi, wakati alipotembelea banda la e-GA katika Maadhimisho ya Kitaifa ya Elimu, Ujuzi na Ubunifu 2024.




Afisa TEHAMA wa e-GA Bi. Khadija Mzenzi, akitoa elimu kuhusu huduma zinazotolewa na e-GA kwa mmoja wa wananchi waliotembelea banda la e-GA wakati wa Maadhimisho ya kitaifa ya Elimu, Ujuzi na Ubunifu.




Afisa TEHAMA wa e-GA Bw. Frank Alex, akitoa elimu kuhusu huduma zinazotolewa na e-GA kwa wananchi waliotembelea banda la e-GA wakati wa Maadhimisho ya Kitaifa ya Elimu, Ujuzi na Ubunifu.



Afisa Habari mwanamizi wa e-GA Bi. Queenter, akitoa elimu kuhusu huduma zinazotolewa na e-GA kwa mmoja wa wananchi waliotembelea banda la e-GA wakati wa Maadhimisho ya kitaifa ya Elimu, Ujuzi na Ubunifu.



Afisa TEHAMA wa e-GA Bw. Claud Charles , akitoa elimu kuhusu huduma zinazotolewa na e-GA kwa wananchi waliotembelea banda la e-GA wakati wa Maadhimisho ya Kitaifa ya Elimu, Ujuzi na Ubunifu.

# KAMATI YA KIUFUNDI YA SERIKALI MTANDAO YAKUTANA



Wajumbe wa Kamati ya Kiufundi ya Serikali Mtandao wakiongozwa na Mwenyekiti wa kamati hiyo Bw.Priscus Kiwango, ambaye pia ni Mkurugenzi wa TEHAMA Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora wakijadili utekelezaji wa Serikali Mtandao wakati kikao kilichofanyika Juni 2024 katika Ofisi za e-GA jijini Dodoma.



Mwenyekiti wa kamati ya kiufundi ya Serikali Mtandao Bw. Priscus Kiwango, akiongoza kikao cha kamati hiyo.



Mjumbe wa kamati ya kiufundi ya Serikali Mtandao Bi Conie Francis, akichangia mada wakati wa kikao cha kamati hiyo.



Wajumbe wa Kamati ya Kiufundi ya Serikali Mtandao wakiwa katika picha ya pamoja mara baada ya kumaliza kikao cha kamati hiyo.

# BODI YA UHARIRI

## MWENYEKITI

Mhandisi Benedict B. Ndomba
Mkurugenzi Mkuu

## WAJUMBE

Salum Mussa
Mkurugenzi wa Huduma na Uwezeshaji

SACP Hamis Ali
Mkaguzi Mkuu wa Ndani

SACP Raphael Rutahiwa
Meneja wa Huduma za Sheria

Long'ida Oltetiai
Meneja wa Huduma kwa Wateja

## MHARIRI

Subira Kaswaga
Meneja Mawasiliano

## WAANDISHI


Catherine Peter | Afisa Habari **Mwandamizi**
Queenter Mawinda | Afisa Habari **Mwandamizi**

## WAPIGA PICHA

Mussa Enock |Afisa Habari
Ben Bago |Afisa Habari

## MSANIFU KURASA

Edger Msamba | Afisa TEHAMA




Ofisi ya Rais,
Mamlaka ya Serikali Mtandao,
Mtumba-Mtaa wa Mtandao.
S.L.P 2833, DODOMA.
+255 26 2961957

Barua pepe: **info@ega.go.tz**
Tovuti: **www.ega.go.tz**